# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1032

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-796-8

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA MBINU ZA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

# STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI

# 2023

HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 1 19/10/2024 14:42

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023

Toleo la Kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-796-8

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kudurufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 2 19/10/2024 14:42

# Yaliyomo


Orodha ya Majedwali ........ iv

Vifupisho ........ v

Shukurani ........ vi

1.0 Utangulizi ........ 1

2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ........ 1

3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu ........ 2

4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu ........ 3

5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 3

6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 5

6.1 Mkufunzi ........ 5

6.2 Mwalimu tarajali ........ 5

6.3 Mzazi/mlezi ........ 6

7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 6

8.0 Zana/vifaa vya Ujifunzaji na Ufundishaji ........ 6

9.0 Upimaji katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 7

10.0 Idadi ya Vipindi ........ 8

11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 8

Bibiografia ........ 36

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na.1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi....................4

Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu....................8

Jedwali Na. 3: Maudhui kwa Mwaka wa Kwanza....................9

Jedwali Na. 4: Maudhui kwa Mwaka wa Pili....................19

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| LAT | Lugha ya Alama ya Tanzania |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 5 19/10/2024 14:42

# Shukurani

Maandalizi ya muhtasari wa somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wakuza mitaala wa TET, wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wataalamu kutoka asasi za kiraia. Vilevile, TET inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndio lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Dkt. Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 6 19/10/2024 14:42

## 1.0 Utangulizi

Somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi, ni moja kati ya masomo ya lazima kwa mwalimu tarajali atakayefundisha somo la Historia ya Tanzania na Maadili ngazi ya Elimu ya Msingi Darasa la III-VI. Maudhui ya somo hili yanalenga kumjengea mwalimu tarajali umahiri wa kumudu maarifa, ujuzi na stadi za mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zitakazomwezesha kufundisha maudhui ya somo la Historia ya Tanzania na Maadili darasa la III-VI, Elimu ya Msingi. Pia, yanalenga kumjengea uwezo wa kutumia teknolojia katika kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji na kutumia njia stahiki za uchopekaji wa masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili. Ufundishaji na ujifunzaji wa somo hili ulenge katika kumwandaa mwalimu tarajali atakayeweza kufikiri, kutafsiri na kutumia mbinu alizojifunza ili kuwezesha mwanafunzi kutafuta maarifa, kujadili, kufanya uchunguzi, kufanya tathimini na kutumia maudhui ya somo la Historia ya Tanzania na maadili katika mazingira yake ya kila siku. Pia, umwezeshe mwalimu tarajali kumudu mbinu za kukuza stadi za karne ya 21 zikiwemo udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini.

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi.

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla.

(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uwajibikaji na lugha ya Taifa.

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma.

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira.

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

Malengo ya Elimu ya Ualimu ni kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu.

(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia.

(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri.

(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi.

(e) Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji.

(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki.

(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji.

(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani classroom-based research).



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 2 19/10/2024 14:42

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu

Umahiri wa jumla wa mafunzo ya stashahada ya ualimu unalenga kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji.

(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia.

(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri.

(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi.

(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji.

(f) Kutambua mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki.

(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji.

(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (instructional leadership).

(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani classroom-based research).

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Muhtasari wa somo la Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi, una umahiri mkuu na umahiri mahususi kama inavyooneshwa katika jedwali namba 1.



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 3 19/10/2024 14:42

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Historia ya Tanzania na Maadili katika Elimu ya Msingi | 1.1 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ujifunzaji na ufundishaji wa Historia ya Tanzania na Maadili<br>1.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili nje ya darasa<br>1.3 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>1.4 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi kabla ya ukoloni<br>1.5 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni<br>1.6 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa la Tanzania katika kipindi cha 1961 hadi sasa<br>1.7 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka<br>1.8 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano kati ya mkufunzi, mwalimu tarajali na mzazi/mlezi katika kutimiza wajibu wao ambao ni:

### 6.1 Mkufunzi

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21.

(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana.

(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao.

(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahik.

### 6.2 Mwalimu tarajali

Mwalimu tarajali anatarajiwa:

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika usimamizi wa darasa na matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji.

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo.

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu.

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji.

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 5 19/10/2024 14:42

### 6.3 Mzazi/mlezi

Mwalimu tarajali anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji.

(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika shughuli za ujifunzaji.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari huu unasisitiza matumizi ya mbinu za ujifunzaji na ufundishaji zinazolenga kumwezesha mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Mkufunzi atatumia mbinu shirikishi kwa kuzingatia mahitaji anuai na uwezo wa mwalimu tarajali katika ujifunzaji. Pia, mbinu zitakazotumika zimwezeshe mwalimu tarajali kufikiri, kutafsiri na kutumia mbinu alizojifunza katika kuwezesha wanafunzi kutafuta maarifa, kujadili, kufanya uchunguzi, kufanya tathimini na kutumia maudhui ya somo la Historia ya Tanzania na maadili katika mazingira yake ya kila siku. Vilevile, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ziwezeshe walimu tarajali kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji na kuchopeka masuala mtambuka wakati wa ufundishaji.

Baadhi ya mbinu za ujifunzaji zinazoweza kutumika ni ziara za kimasomo, midahalo, klabu za masomo, utafutaji wa taarifa za historia, tafiti ndogo, matumizi ya vyanzo vya historia, matumizi ya nyaraka, uchunguzi, majadiliano, masimulizi, kisamafunzo, igizodhima, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi) na kazi nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji na ufundishaji wa somo hili.

## 8.0 Zana/vifaa vya Ujifunzaji na Ufundishaji

Zana/vifaa vya ujifunzaji na ufundishaji zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji na uwezo wa mwalimu tarajali. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha mwalimu tarajali anapata nafasi ya ama kuona, kusikia na kushika zana wakati wa ujifunzaji na ufundishaji. Pia, zana na vifaa vya ujifunzaji na ufundishaji vinapaswa vimsaidie mwalimu tarajali kumudu kinachofundishwa. Mkufunzi anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzunguka. Vilevile, mkufunzi atumie vitabu vya kiada, ziada



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 6 19/10/2024 14:42

na vifaa vingine vya ufundishaji na ujifunzaji vilivyopata ithibati ya Taasisi ya Elimu Tanzania (TET). Baadhi ya zana na vifaa vitakavyotumika kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji vimependekezwa katika jedwali la maudhui katika safu ya zana/vifaa.

## 9.0 Upimaji katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Upimaji ni suala muhimu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji ili kuwezesha ujenzi wa umahiri unaokusudiwa. Upimaji wa Somo la Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji ili kumwezesha mkufunzi kubaini uwezo na uhitaji wa mwalimu tarajali katika ujifunzaji na kisha kumwezesha kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa umahiri wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili Elimu ya Msingi. Pia, upimaji uwezeshe umahiri wa mwalimu tarajali kumudu stadi za kuchopeka masuala mtambuka, kuratibu shughuli nje ya darasa na kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika katika upimaji endelevu ni bungua bongo, orodha hakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi, mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo.

Upimaji tamati utahusisha mitihani na majaribio ya mwezi, mihula na mtihani wa mwisho wa mwaka. Aidha, taarifa za upimaji huu pamoja na kutumika katika kutathimini maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji, zitatumika kama mrejesho wa kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji.

Katika kuamua kiwango cha ufaulu wa mwalimu tarajali upimaji wa mwisho (tamati) utachangia asilimia sabini (70%) na upimaji endelevu utachangia asilimia thelathini (30%). Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia hamsini (50%) na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafikisha asilimia hamsini (50%), mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama katika upimaji endelevu.

**Jedwali Na. 2:** *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu*

| Na | Shughuli ya Upimaji | Mgawanyo (%) |
|---|---|---|
| 1 | Mitihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 2 | Mitihani wa Mwisho wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 3 | Mitihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Pili | 6.0 |
| 4 | Kazi mradi | 7.0 |
| 5 | Mkoba wa kazi | 5.0 |
| | **Jumla** | **30** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji wa Historia ya Tanzania na Maadili, unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ujifunzaji na ufundishaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni saa moja (1). Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi vitano (5) kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari wa Mbinu za Ujifunzaji na Ufundishaji wa Historia ya Tanzania na Maadili umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele sita ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, vifaa/zana pamoja na idadi ya vipindi kama Jedwali namba 3 na 4 linavyoonesha.



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 8 19/10/2024 14:42

## Mwaka wa Kwanza

**Jedwali Na 3:** *Maudhui ya Mwaka wa Kwanza*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Historia ya Tanzania na Maadili katika Elimu ya Msingi | 1.1 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ujifunzaji na ufundishaji wa Historia ya Tanzania na Maadili | (a) Kumudu ufaraguzi wa vifaa saidizi sahili katika ujifunzaji na ufundishaji wa Historia ya Tanzania na Maadili | Mwalimu tarajali amemudu ufaraguzi wa vifaa saidizi sahili katika ujifunzaji na ufundishaji wa Historia ya Tanzania na Maadili | - Kompyuta, simu, tableti, projekta<br>- Makunzi yanayopatikana katika mazingira yake<br>- Manila kadi, matini, ramani, chati picha/picha mguso | 30 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ujifunzaji na ufundishaji wa Historia ya Tanzania na Maadili | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ujifunzaji na ufundishaji wa Historia ya Tanzania na Maadili | - Kompyuta, simu, tableti, projekta<br>- Makunzi yanayopatikana katika mazingira yake<br>- Matini zenye maudhui yanayohusu historia ya Tanzania na maadili | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili nje ya darasa | (a) Kumudu matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili nje ya darasa | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili nje ya darasa | - Chati pindu, filamu na matini zinazohusu mbinu na mikakati ya kuratibu shughuli za ujifunzaji na ufundishaji nje ya darasa | 35 |
| | 1.3 Kumudu matumizi ya mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya sanaa na michezo *(mfano hadithi, nyimbo, igizodhima, majigambo nk)* katika ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za | - Filamu zenye maudhui yanayohusu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji<br>- Picha zenye vifaa, bidhaa na teknolojia ya jamii za kale<br>- Matini/picha/picha mguso/chati zenye maudhui yanayohusu maendeleo na maadili ya Kitanzania kabla ya ukoloni | 35 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kitanzania kabla ya ukoloni | | |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni katika darasa kubwa | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu anuai za ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni katika darasa kubwa | - Matini/picha/ picha mguso/filamu zinazoonesha maendeleo ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>- Nyimbo na hadithi<br>- Filamu/picha/chati/ matini zenye mbinu na mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji katika darasa kubwa | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji | - Matini /picha/filamu zinazohusu maendeleo ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>- Picha zenye masuala mtambuka | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 11 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | - Maudhui ya mbinu mbalimbali za ujifunzaji wa maudhui ya masuala mtambuka zilizoifadhiwa kwenye midia<br>- Visa mafunzo vinavyohusu masuala mtambuka | |
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | - Kompyuta, tableti na simu, video, projekta<br>- Tovuti na filamu zenye mada zenye maudhui ya maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania<br>- Filamu zenye makala za mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu nyinginezo *(Mfano mdahalo, masimulizi, igizodhima, ziara za kimasomo, uchunguzi, matumizi ya nyaraka za kihistoria, matumizi ya vyanzo vya historia, onesho mbinu, fikiri-andika-jozisha-shirikisha, maswali na majibu, majadiliano nk)* za ujifunzaji na ufundishaji wa | - Matini yenye mbinu za ufundishaji na ujifunzaji<br>- Matini/picha/picha mguso/chati zenye maudhui yanayohusu maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 13 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni | | |
| | 1.4 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi kabla ya ukoloni | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya sanaa na michezo *(mfano nyimbo, hadithi, igizodhima, picha)* katika ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi | - Matini yenye picha, nyimbo zinazohusu ushirikiano baina ya jamii<br>- Filamu zinazohusu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji | 35 |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 14 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi katika darasa kubwa | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu anuai za ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi katika darasa kubwa | - Matini yenye picha, nyimbo zinazohusu ushirikiano baina ya jamii<br>- Nyimbo na hadithi<br>- Filamu/picha/chati/ matini zenye mbinu na mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji katika darasa kubwa | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 15 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi | - Matini zenye masuala mtambuka<br>- Maudhui ya mbinu mbalimbali za ujifunzaji wa maudhui ya masuala mtambuka zilizoifadhiwa kwenye midia<br>- Visa mafunzo vinavyohusu masuala mtambuka<br>- Picha/picha mguso zenye bidhaa na vifaa walivyobadilishana jamii | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 16 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kuchopeka TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi | - Kompyuta, tableti na simu, video, projekta<br>- Maudhui yanayohusu ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania yaliyoifadhiwa katika midia<br>- Filamu zenye makala za mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 17 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu nyinginezo *(mfano uhalisishaji wa tukio, kisa mafunzo, maswali na majibu, utafiti mdogo, masimulizi, mdahalo, matumizi ya nyakara za kihistoria, majadiliano, bunguabongo nk)* za ujifunzaji na ufundishaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi | - Matini yenye mbinu za ufundishaji na ujifunzaji<br>- Matini/picha/picha mguso/chati zenye maudhui yanayohusu ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 18 19/10/2024 14:42

## Mwaka wa Pili

**Jedwali Na.** ***4*****:** *Maudhui ya Mwaka wa Pili*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa Historia ya Tanzania na Maadili katika Elimu ya Msingi | 1.5 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya sanaa na michezo *(mfano hadithi, majigambo, nyimbo, igizodhima)* katika ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni | - Manila kadi, matini, ramani, chati zenye kuonesha mifumo ya kikoloni<br>- Picha/picha mguso zinazoonesha ukoloni wakati na baada ya ukoloni<br>- Filamu/picha zenye mbinu za matumizi ya sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji | 65 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu anuai za ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati | - Ramani na chati yenye kuonesha mifumo ya kikoloni<br>- Picha/matini/filamu zanye taarifa za ukoloni<br>- Filamu/picha/chati zenye mbinu na mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji katika darasa kubwa | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 19 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ukoloni katika darasa kubwa | wa ukoloni katika darasa kubwa | - Matini yenye maudhui ya mbinu na mikakati ya kumudu ufundishaji darasa kubwa | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleona maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni | - Picha zenye masuala mtambuka<br>- Maudhui ya mbinu mbalimbali za ujifunzaji wa maudhui ya masuala mtambuka<br>- Visa mafunzo vinavyohusu masuala mtambuka<br>- Ramani, chati yenye mifumo ya kikoloni, picha | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni | - Kompyuta, tableti na simu, video, projekta<br>- Tovuti na filamu zenye mada zenye maudhui ya maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania<br>- Maudhui yanayohusu maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati na baada ya ukoloni zilizoifadhiwa kwenye midia<br>- Filamu zenye makala za mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 21 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu nyinginezo *(mfano mdahalo, masimulizi, changanyakete, ziara za kimasomo, uchunguzi, matumizi ya nyaraka za kihistoria, onesho mbinu, fikiri-andika-jozisha-shirikisha, maswali na majibu, majadiliano nk)* za ujifunzaji na ufundishaji wa maendeleo na maadili ya jamii za | - Matini /picha/picha mguso/ chati zenye maudhui yanayohusu maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati na baada ya ukoloni<br>- Filamu/picha zenye mbinu za ufundishaji na ujifunzaji | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 22 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kitanzania wakati wa ukoloni | | |
| | 1.6 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa | - Manila kadi, matini, chati, picha, picha mgusu zenye maudhui ya historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa<br>- Filamu/picha zenye mbinu za matumizi ya sanaa na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji<br>- Nyimbo za Taifa na kizalendo | 80 |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 23 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa katika darasa kubwa | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu anuai za ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa katika darasa kubwa | - Matini na takwimu zinazohusu historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa<br>- Picha/picha mguso, ramani, chati zenye historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa<br>- Filamu/picha/chati zenye mbinu na mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji katika darasa kubwa<br>- Matini yenye maudhui ya mbinu na mikakati ya kumudu ufundishaji darasa kubwa | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 24 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa | - Matini zenye maudhui ya masuala mtambuka<br>- Picha, ramani, chati ya mifumo iliyojengwa mwanzoni wa uhuru 1961-1966<br>- Visa mafunzo vinavyohusu masuala mtambuka<br>- Nyimbo na picha zenye masuala mtambuka | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 25 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa | - Matini zenye maudhui na takwimu za historia na maadili ya ujenzi wa Taifa kuanzia 1961 hadi sasa zilizoifadhiwa katika midia<br>- Kompyuta, tableti na simu, video, projekta<br>- Tovuti na filamu zenye mada zenye maudhui ya historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa<br>- Filamu zenye makala za mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu nyinginezo *(mfano mdahalo, masimulizi, changanyakete, ziara za kimasomo, uchunguzi, matumizi ya nyaraka za kihistoria, onesho mbinu, majadiliano nk)* za ujifunzaji na ufundishaji wa historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa | - Matini na takwimu zinazohusiana na historia na maadili ya ujenzi wa Taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa<br>- Filamu/picha zenye mbinu za ufundishaji na ujifunzaji | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 27 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.7 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya sanaa na michezo *(mfano nyimbo, majigambo, igizodhima, picha, hadithi)* katika ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka | - Matini mbalimbali, zenye sanaa na michezo<br>- Filamu zenye matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji | 45 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka katika darasa kubwa | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu anuai katika ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka | - Matini yenye maudhui yahusuyo maarifa ya jamii<br>- Nyimbo na hadithi<br>- Filamu/picha/chati/matini zinazohusu mbinu na mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji katika darasa kubwa | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 28 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | katika darasa kubwa | | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kuchopeka maswala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka | - Picha zenye masuala mtambuka<br>- Maudhui ya mbinu mbalimbali za ujifunzaji wa maudhui ya masuala mtambuka zilizoifadhiwa kwenye midia<br>- Visa mafunzo vinavyohusu masuala mtambuka<br>- Matini zenye maudhui yanayohusu maarifa ya jamii | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 29 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka | - Kompyuta, tableti na simu, video, projekta<br>- Maudhui yanayohusu maarifa ya jamii yaliyoifadhiwa katika midia<br>- Filamu zenye makala za mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 30 19/10/2024 14:42

| **Umahiri mkuu** | **Umahiri mahususi** | **Shughuli za ujifunzaji** | **Vigezo vya upimaji** | **Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu nyinginezo *(mfano, utafiti, kisa mafunzo, masimulizi, mdahalo, maswali na majibu, matumizi ya nyakara za kihistoria, majadiliano, ziara za kimasomo nk)* za ujifunzaji na ufundishaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka | - Matini/filamu yenye mbinu za ufundishaji na ujifunzaji<br>- Matini zenye maudhui yanayohusu maarifa ya jamii | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 31 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.8 Kumudu mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania | (a) Kumudu matumizi ya sanaa na michezo katika ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya sanaa na michezo *(mfano nyimbo, majigambo, igizodhima, picha)* katika ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania | - Filamu zenye mbinu za ujifunzaji na ufundishaji kwa kutumia michezo na sanaa<br>- Matini/chati zenye maudhui yanayohusu ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania<br>- Vifaa vya urithi na utamaduni | 30 |
| | | (b) Kumudu matumizi ya mbinu anuai za ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania katika darasa kubwa | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu anui katika ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili | - Visa mafunzo vinavyohusu ulinzi wa historia, urithi na maadili<br>- Filamu/picha/chati/ matini zenye mbinu na mikakati ya ufundishaji na ujifunzaji katika darasa kubwa | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | ya Tanzania katika darasa kubwa | | |
| | | (c) Kumudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kuchopeka masuala mtambuka katika ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania | - Matini zenye maudhui ya masuala mtambuka<br>- Maudhui ya mbinu mbalimbali za ujifunzaji wa maudhui ya masuala mtambuka<br>- Matini zenye maudhui yanayohusu ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 33 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kumudu matumizi ya mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania | - Kompyuta, tableti na simu, video, projekta,<br>- Matini yahusuyo ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania yaliyoifadhiwa kwenye midia<br>- Mbinu za kutumia TEHAMA katika ujifunzaji na ufundishaji zilizoifadhiwa katika midia | |



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 34 19/10/2024 14:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kumudu matumizi ya mbinu nyinginezo za ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania | Mwalimu tarajali amemudu matumizi ya mbinu nyinginezo, *(mfano ziara za kimasomo, onesho mbinu, midahalo kisa mafunzo, utafiti mdogo, matumizi ya nyaraka, uchunguzi, bunguabongo changanyakete, matembezi ya galari)* katika ujifunzaji na ufundishaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania | - Picha/picha mguso au matini yenye maudhui ya ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania<br>- Filamu zenye makala yenye mbinu za ujifunzaji na ufundishaji wa historia, urithi na maadili | |

## Bibiografia


Burton, W. H. (2021). *Principles of History Teaching.* Routledge

David, Newble & Robert, Cannon (1995). *A Handbook for teachers in the University and College: A Guide to improving teaching methods*. Kogan Page

Doppen, Frans H. (2004). "Beginning Social Studies Teachers' Integration of Technology in the History Classroom," *Theory and Research in Social Education*, Vol. 32, No. 2 pp.248-279.

Garrett, Tracey. (2008). "Student-Centered and Teacher-Centered Classroom Management: A Case Study of Three Elementary Teachers", *Journal of Classroom Interaction*, Vol. 43, No. 1 pp. 34-47.

Harris, E. (2007). "How can Teachers put competency-based curricula into Practice?" *Journal of Initial Teacher Inquiry,* Vol. 3 pp. 12-15.

Kafyulilo A.C, B.I Rugembuka & I. Moses. (2015) "The implementation of competency-basedteaching approaches in Tanzania," *Makerere Journal of Higher Education*, Vol. 4,No.2. pp.311-326.

Komba & Mwandanji. (2015). "Reflections on the implementation of competence-based curriculum in Tanzanian secondary schools," *Journal of Education Learning*, Vol.4, No.2. pp.73-79.

Lawi, Y.L . (1996). "Towards an understanding of the basic problems in the teaching of History in post-colonial Tanzania" *Tanzania Zamani,* Vol. 1. No.4. pp. 1-9.

Maloy, R, W. & Irene S. L. (2010). "Student-Centered Teaching Methods in the History Classroom: Ideas, Issues and Insights for New Teachers," *Social Studies Research and Practice*, Vol. 5, No. 3 pp. 46-61.




HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 36 19/10/2024 14:42

Moodley, P. (2015). Student overload at university: large class teaching challenges: part 1. South African *Journal of Higher Education, 29 (3), 150-160*

Mugabe, L. & Ndayambaje, I. (2022). The implications of large classes on active learning at University of Rwanda-college of Education. *Rwandan Journal of Education, vol. 5, No. 2*

Ndomondo Eunice, Akundael Mbise and Joviter Katabaro. (2022). "History Teachers' conceptualization of competency-based curriculum in transforming instructional practices in lower secondary schools in Tanzania," *Social Sciences and Humanities*, Vol.6 No. 1.

Olajide, J.O. (2012). Teaching Science for Better Achievement in Large Classes. *International Journal of African studies*

Oyewale, Gbemisola Mary Oyewale and Jonathan Oluropol Familuga. (2021). "The Use of Technology in Teaching and Learning of History in Secondary Schools," *American Journal of Multidisciplinary Research & Development*, Vol.3, No.6. pp.43-48.

Stephens, Robert P. et.al., (2005). "Using Technology to Teach Historical Understanding: the Digital History Reader Brings the Possibilities of New Technology to the History Classroom," *Social Education,* Vol. 69, No.3.

Zhang, J. (2002). The survey and analysis of big class English teaching. *Journal of North China* Institute of Water Conservancy and Hydroelectric Power (Social Sciences Edition), 18(4), 92-94

Zhang, L. (2010). Problems of teaching English in primary large classes in rural areas and application of group study. *Journal of Guangxi Normal University for Nationalities, 27(1), 129-131*

Zhang, L. (2010). Problems of teaching English in primary large classes in rural areas and application of group study. *Journal of Guangxi Normal University for Nationalities, 27(1), 12*



HISTORIA YA TZ NA MAADILI 2.indd 37 19/10/2024 14:42